BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Ishirini – Tarehe 3 Juni, 2017.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

71. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

Pamoja na Wizara kutoa ahadi katika Baraza la Nane kufanyia matengenezo mtaro wa eneo la Mnadani Darajani, miaka mitatu sasa imepita tokea ahadi ile itolewe mtaro ule haujafanyiwa matengenezo. Mhe. Waziri alimpeleka aliyekuwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa wakati ule ambaye sasa ni Mkuu wa Wilaya Micheweni lakini agizo lile halijatekelezwa.

(a) Kwanini Wizara haijatekeleza ahadi yake ya kufanyia matengenezo mtaro ule kama ilivyoahidi Barazani.

(b) Hatua gani za haraka zitachukuliwa baada ya kuikumbusha Wizara ili mtaro ule utengenezwe.

(c) Kutotekelezwa ahadi ile Wizara haioni kuwa imelidanganya Baraza au kulidharau.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

187. MHESHIMIWA MOHAMMED SAID MOHAMMED (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha mradi wa kubadilisha nyaraka kutoka mfumo wa kutumia karatasi "manual" kwenda katika mfumo wa kielektroniki.

(a) Je, vifaa vilivyotumika vina uhakika gani wa kuacha nyaraka katika uhalisia wake.

(b) Je, kuna uhakika wa kuzitumia rekodi za elektoroniki inavyotakiwa.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

155. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi katika kuendeleza elimu na kufikia kiwango cha juu katika sekta hii kwa kuleta vitabu na vifaa vya kila aina vya kukuza elimu. Lakini bado Pemba katika ghala la elimu la kuhifadhia vitabu Chake Chake hali imekuwa mbaya na kutothamini juhudi za Serikali za kuleta vifaa hivyo na kuviweka katika eneo sio stahiki.

(a) Je, Serikali inalijua hilo.

(b) Ghala hilo la kutunza vitabu limekodiwa na Serikali au tumesaidiwa.

(c) Hatuoni hali ile ya ghala ya vitabu kuharibika kwa vitabu ni kulitia hasara Taifa.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

16. MHESHIMIWA HIDAYA ALI MAKAME (Nafasi za Wanawake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa kuwa Kilimo ni uti wa mgongo kwa maendeleo ya mwanadamu na ili kukiendeleza kilimo, Wizara ya Kilimo inasisitiza zaidi juu ya kilimo cha umwagiliaji ambapo wananchi wanatekeleza wajibu wao kwa kufuata maelekezo ya Wizara na wahusika wake (mabwana shamba).

(a) Je, wananchi ambao wanaolima kilimo hicho cha umwagiliaji na kukiacha kilimo cha asili cha kufuata miongo ya mwaka wanapopatwa na maafa mbali mbali kama vile mabonde kujaa maji wakati wa masika na mazao kufukiwa na maji na kupotea, Wizara huwasaidia vipi.

(b) Je, wananchi hawa ambao wanapatwa na maafa hayo kila mwaka hususan mabonde ya Kizimbani, Mkanyageni, Bubwisudi na Miwani watakuwa na imani gani na kilimo cha umwagiliaji pamoja na kufuata ushauri wa Wizara endapo watakuwa hawasaidiwi wanapopatwa na maafa.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

113. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Serikali ya Zanzibar inajitahidi kuimarisha suala la maji lakini mpaka leo maji hayo hayatoshelezi kwa matumizi na hayana ubora wa kunywa hali inayosababisha viwanda vya maji kuongezeka.

(a) Je, ni lini sekta ya maji itatosheleza matumizi ya maji Zanzibar.

(b) Je, ni lini maji hayo yatakuwa salama kwa kiwango kinachokubalika kwa matumizi ya kunywa bila matatizo ya afya.

(c) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa kuvilinda vyanzo vya maji ambavyo kwa muonekano wa wazi vyanzo hivyo vinapotea.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

44. MHESHIMIWA ABDALLA MAULID DIWANI (Jimbo la Jang'ombe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanzisha Idara ya Usafirishaji na Ukanguzi wa Magari na Vyombo vyengine vya Moto, Hata hivyo, kumekuwa na usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaohitaji huduma katika Idara hiyo pale Karakana ambapo ametaka huduma hulazimika kwenda Karakana na kwenda kufanya malipo Bank na kisha kurejea tena Karakana.

(a) Je, hatuoni kama tunaongeza usumbufu katika utoaji wa huduma hizo.

(b) Ni sababu zipi zilizofanya ishindikane kuweka mfanyakazi wa PBZ pale Karakana kwa kukusanya mapato ya huduma hizo ili kuondoa usumbufu huo.

143. MHESHIMIWA DKT. MWINYIHAJI MAKAME MWADINI (Jimbo la Dimani) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kwa miaka mingi ya nyuma barabara kuanzia Forodhani kupitia jengo la Wizara ya Kilimo la zamani kwendea Kiponda na kutokezea Darajani kwa Muzamil ilikuwa inatumika kwa gari ndogo. Pia barabara itokayo Msikiti wa Ijumaa Malindi kupitia jengo lililokuwa la Wizara ya Mawasiliano Jamatini hadi Darajani ilikuwa nayo ikitumika.

(a) Ni sababu zipi za msingi zilizopelekea barabara hizo kutotumika hivi sasa.

(b) Je, Wizara haioni kama barabara hizo zikitumika baada ya matengenezo zitatanzua tatizo la msongomano wa gari liliopo hivi sasa hapo Malindi.

Wizara ya Afya:

119. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa kuna wanafunzi waliomaliza mafunzo ya udaktari kwenye darasa la Wacuba mwaka 2016 ambao walitokea Unguja na Pemba ambapo kati yao vijana sita kutoka Unguja wameshaajiriwa mwezi wa Machi, 2017.

(a) Je, ni kwa sababu gani wakaajiriwa vijana hao wote 6 kutoka Unguja.

(b) Je, ni kwa sababu gani wasiajiriwe vijana watatu kutoka Pemba na watatu kutoka Unguja, mara ya kwanza na mara ya pili wakaendelea kumalizia wengine ili kupunguza manung'uniko yaliyopo kwamba wameajiriwa vijana hao kutoka Unguja tu.

II. HOJA ZA SERIKALI

Waziri wa Afya:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka 2017/2018.

Zanzibar,
3 Juni, 2017.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.